

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

Simu: +255 026 23222761-5

Fax No. +255 026 2322624

E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Spika wa Bunge, Mheshimiwa Job Ndugai (Mb) ameamuru Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima na Mheshimiwa Jerry William Silaa kupelekwa mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili kujibu tuhuma mbalimbali ikiwemo kusema uongo na kushusha hadhi na heshima ya Bunge.

Waheshimiwa hao wanatakiwa kufika mbele ya Kamati hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 4 (1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 ambayo inaipa mamlaka Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuchunguza mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yanayopelekwa na Spika.

Mheshimiwa Josephat Gwajima anatakiwa kufika mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Jumatatu tarehe 23 Agosti, 2021 saa saba kamili (7:00) Mchana katika ukumbi namba 229, Jengo la Utawala lililopo katika Ofisi ya Bunge Dodoma.

Mheshimiwa Jerry Silaa anatakiwa kufika mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Jumanne tarehe 24 Agosti, 2021 saa saba kamili (7:00) Mchana katika ukumbi namba 229 Jengo la Utawala lililopo katika Ofisi ya Bunge Dodoma.

Endapo yeyote kati ya Waheshimiwa waliotajwa hatafika mbele ya Kamati kwa siku na muda uliotajwa, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa kifungu cha 17 na 34 (1) (a) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296, Toleo la Mwaka 2020.

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
DODOMA.

21 Agosti 2021.